Taarifa ya wiki ya nenda usalama barabarani mkoa wa Mbeya
28 septemba – 3 oktoba 2009

Tulisafiri salama kutoka Dar mpaka Mbeya. Tarehe 25 septemba tulifika ofisi ya usalama mkoa wa Mbeya RTO Mr Mgeni, alitoa ushirikiano mzuri kutushauri na kutuelekeza namna ya kuwapata wanafunzi wanaotumia baisikeli kwenda shuleni.

Tulifika shule ya Muungano pamoja na shule ya Manga zito zipo mjini Mbeya na wanafunzi hugongwa sana wakati wanaenda shuleni. Walimu wao walifurahi sana kusikia UWABA wanatoa elimu ya usalama barabarani wanapoendesha baisikeli. Tulishauriwa kutoa elimu hiyo uwanjani ili watu wote waweze kuona ni namna gani UWABA inavyotoa elimu ya wapanda baisikeli. Na kila tulichokuwa tunafundisha walikuwa wanakirekodi.

Wiki ya nenda usalama barabarani ilifunguliwa rasmi katika uwanja wa mwanjerwa mkoani Mbeya tarehe 28.9.2009. Mgeni rasmi Naibu Waziri kiongozi kutoka Zanzibar Mhe Ally Juma Shamuhuna. Alipofika kwenye banda letu alifurahishwa na kazi ya UWABA kutoa elimy ya usalama wa wapanda baisikeli hasa elimu hiyo kuanzia watoto wa shule na alipendekeza na Zanzibara tupeleke elimu hiyo ya usalama barabarani kwa wapanda baisikeli. Mgeni rasmi tulimukasithi mwongozo wa baisikeli pamoja na kanuni za sheria barabarani alitupongeza sana. Tarehe 29.9.2009 watu walikuwa wengi sana kwenye wanaohitaji elimu tulijigawa Sosthenes alibaki kibandani akiendelea kutoa elimu na Dominata nilitembelea maeneo yanayozunguka uwanja wa Mwanjerwa na kuwafundisha elimu ya usalama barabarani kwa wapanda baisikeli na wanaokodisha baisikeli ili wazijue sheria za usalama barabarani. Kazi ilikuwa kubwa mno kwani kila mtu anahitaji elimu hiyo sababu watu hawakuwahi kuelimishwa juu ya usalama barabarani kwa wapanda baisikeli.

Watu waliendelea kufika kwenye bande letu kila siku mnatoa elimu mpaka sauti inakauka.

Tarehe 30.9.2009 tulianza elimu ya usalama barabarani kwa wanafunzi wanatumia baisikeli shuleni walikaa makundi ili waweza kuzijua sheria kanuni pamoja na kuweza kujibu maswali. Tarehe 1.10.2009 tuliendelea na wanafunzi wa shule na kuwapeleka barabarani kwenye makutano ya barabara ili waweze kuelewa zaidi shereia za barabara wanafunzi walielewa vizuri na walikuwa wasikivu na kutoa ushirikiano na somo la baisikeli walipenda sana.

Tarehe 2.10.2009 tuliendelea na kutoa elimu kwa watu wote waliofika kwenye banda letu.

Tarehe 3.10.2009 maazimisho ya usalama barabarani yalifunwa na mgeni rasmi alikuwa Mkuu wa Mkoa wa Mbeya Mhe Jhoni Mwakipesile. Alitembelea mabanda yote. Kwenye banda letu alikutana na wanafunzi ambao tayari wameshaijua sheria ya usalama barabarani kwa wapanda baisikeli wameralia helmet pamoja na reflecta jaketi walipita kwa mgeni rasmi wakiwa na baisikeli zao kwa kuendesha msatari mmoja watu walishangilia sana. UWABA tulikuwa kuvutio kikubwa kwani hawakuwahi kuona elimu ya usalama barabarani kwa wapanda baisikeli. Maonyesho hayo tulikuwa kitu kipya. Tulitoa zawadi ya reflecta jaketi pamoja na helmet kwa mgeni rasmi alifuarishwa na zawadi. UWABA vile vile tulitoa zawadi ya reflecta jaketi pamoja na helmet kwa baraza la taifa la usalama barabarani Tanzania. Walitupongeza sana. Mgeni rasmi alitoa cheti kimoja kwa niaba ya wanafunzi wote waliohitimu mafunzo ya sheria ya usalama barabarani kwa wapanda baisikeli. Hotuba ya mgeni rasmi alipongeza UWABA kwa kutoa elimu ya usalama barabarani kwa wapnda baisikeli na kusema elimu iwe endelevu kwani ni watu wenye hawajui sheria za barabarani na baisikeli ni chombo cha usafiri ambacho kina watumiaji wengi vijijini na mjini.

Ushauri wa mgeni rasmi – vyeti vya UWABA vigongwe muhuri na kuvibainingi ili viwe ubor zaidi.

Mashirika yaliyoshiriki wiki ya nenda usalama barabarani:

- UWABA
- Amend
- Miundombinu (TANROADS)
- TBS
- Jeshi la polisi usalama barabarani
- TAMESA
- VETA
- Baraza la taifa la usalama barabarani
- Scania
- SGS
- SUMATRA
- Ushauri nasaa na VVU
- Tigo
- Kikosi cha zimamoto
- Kikosi cha kuzuia madawa ya kulevya

Mapendekezo
Muda umefika wa UWABA kutafuta pesa za kushiriki wiki ya nenda usalama barabarani mwaka 2010 kunua vifaa vya UWABA kama turubai ubao wa kuweka matangazo, kuchapisha vipeperushi, vinavyoonyesha kazi za UWABA, kuwa na pesa za kukodi meza na viti wakati wa kushirik, kucahptisha mwongozo wa kutosha pamoja na kanuni, reflecta jaket na helmet vipatikane kwa wingi ni pamoja na vya kuuza kwani mikoani ni shida kubwa kuvipata, hivyo walipendekeza kama tunaweza kuwauzia.

Posho ziongezwe kwa washiriki kwani gharama za mikoani zinabadilika. Hotel ya Tsh 5,000 haina usalama hotel yenye usalama ni kuanzai Tsh 15,000 na kuendelea. Vyakula kuanzia Tsh 3,500 na kuendelea inabidi kushirikana kutafuta wafadhili kufanya kazi kwa usanifu.

Shukrani
Tunawashukuru Amend kwa ushirikiano wa Turubai wasingekuwepo tusingeweza kushiriki au tungekodi pesa kubwa sana kitu ambacho kisingewezekana kwani pesa tulikuwa hatuna.

Tunamshukuru RTO wa Mkoa wa Mbeya Mr Mbeni alitoa ushirikano mkubuwa kwa ushauri wa wanafunzi pamoja na mabo ya viti na meza.

Maombi
Tuwaombe ofisi ya kamanda Kombe atupe CD ya usalama barabarani kwani walikuwa wakirekodi kila kilichofanyika cha UWABA hivyo itatusaidia kuboresha zaidi kazi zetu.

Taarifa hii imeandikwa na Mr Sosthenes C Amlima, Mrs Dominata Rwechungura. Tunawashukuru kwa kutuchagua kuwakilisha UWABA mkoa wa MBeya. Tunaomba kuwasilisha.